

# Wananchi na uchu wa mabadiliko

## Je, wananchi wanashiriki na wanaweza kuiwajibisha Serikali?









## 1. Utangulizi

Demokrasia iliyo hai na inayotekeleza kazi kwa ufanisi inahitaji wananchi huru ,wenye uchu wa kushiriki katika mabadiliko ya nchi na wenye uwezo wa kujadili na kushawishi mambo muhimu, kuwajibisha Serikali na kuchukua hatua wenyewe. Hata hivyo, uwezo wa raia kujituma huwa unazimwa au kusongwa na vikwazo, vikiwemo vikwazo vya nje (dola kuzuia uhuru wa kushiriki) au vikwazo vyake mwenyewe (kwa kujihisi kuwa yeye binafsi hana uwezo).

Katika muhtasari huu, tunachunguza mambo mawili: hisia za wananchi zenye uwezo wa kuleta msukumo utaochochea matokeo yanayotakiwa (imani katika uwezo wa mtu mwenyewe kuwa anaweza kufanikisha malengo yake), vile vile namna ambayo wananchi wanachangamana wenyewe kwa wenyewe na viongozi wenye mamlaka. Ni kwa kiasi gani Watanzania pamoja na wawakilishi wa Serikali wanatumia majukwaa yaliyopo au majukwaa mapya kujadili masuala mbali mbali? Na ni kwa kiasi gani jamii tofauti tofauti zinaaminiana? Pia je, imani hii inajidhihirisha katika ushiriki wa jamii katika uchukuaji hatua?

Muhtasari huu unaripoti takwimu zenye uwakilishi wa kitaifa juu ya mitazamo ya wananchi katika kuaminiana na kujituma. Takwimu zimetokana na awamu ya 20 ya Sauti za Wananchi, utafiti wa kwanza Afrika wenye uwakilishi wa kitaifa (www.twaweza.org/sauti). Takwimu zilikusanywa kupitia simu zilizopigwa kwa washiriki 1,405 kutoka Tanzania Bara kati ya tarehe 27 Juni na tarehe 10 Julai, 2014.

Matokeo Muhimu ya muhtasari huu ni:

- Watanzania wanaamini zaidi viongozi wa dini (87%), Rais (71%), pamoja na ndugu zao (88%).
- Imani kwa jamii ni kubwa sana: karibu watu wote (98%) wanaamini kuwa jamii ina uwezo wakuungana iwapo tukio baya litatokea.
- Ushiriki katika jamii ni mkubwa: wananchi 72% wamejiunga na mashirika ya kijamii, kwa mfano makundi ya kidini au makundi ya kuweka na kukopa pamoja na vikundi vya mikopo.

Muhtasari huu umeandaliwa na Uwazi - Twaweza, iliyopo Hivos Tanzania.
Wachangiaji ni Elvis Mushi, Youdi Schipper na Angela Ambroz. Takwimu zilikusanywa na asasi ya Ipsos Tanzania. Imetolewa mwezi Septemba 2014.

S.L.P 38342, Dar es Salaam, Tanzania.
Simu: +255 22 266 4301 | barua pepe: uwazi@twaweza.org
www.twaweza.org/sauti

Twaweza ni sisi

- Takriban nusu ya Watanzania hawajawahi kuongea na mwenyekiti wao wa mtaa au hata wa kijiji.

# 2. Mambo nane kuhusu uwezo wa raia kujituma


## Jambo la 1: Watanzania wanayo imani na jamii yao

Walipoulizwa ni kwa kiasi gani uaminifu upo kati ya watu mbalimbali, wananchi waliripoti kuwa wana imani zaidi na viongozi wa dini (87% "kwa kiasi fulani" au "sana") pamoja na ndugu zao kwa kiasi karibu sawa na ile cha viongozi wa dini (88%). Ingawa watu hawakuonesha kuwepo kwa uaminifu mkubwa kwa wanasiasa, Rais alionekana kuaminiwa na zaidi ya nusu ya wananchi (71%). Kwa ujumla, wananchi walionesha imani na watu walio karibu nao zaidi ikiwa kwa wastani, watu 8 kati ya 10 walioripoti kuwa na imani na majirani zao (76%) na ndugu (88%) "sana" au "kwa kiasi fulani" (Kielelezo cha 1).

Wananchi pia walionesha kuwa na imani kwa watoa huduma katika ngazi za kijamii/mitaa. Watu 7 kati ya 10 waliripoti kuwa wana imani na walimu wakuu (71%), na waliripoti kuwa hata wafanyakazi vituo vya afya (68%) waliweza kuaminiwa "sana" au "kwa kiasi fulani". Hata hivyo, nusu ya wananchi waliosema wasambazaji maji wanaweza kuaminika.

Pia kulikuwa na imani kubwa katika mitandao ya usalama ndani ya jamii: wananchi walipoulizwa iwapo tukio baya, au tukio lisilotarajiwa (kama vile nyumba kuungua moto), je, jamii ingekusanyika kusaidia? Watanzania 98% walijibu ndiyo. Asilimia 18% kati yao walisema "uwezekano upo" na 80% walisema "uwezekano mkubwa sana ulikuwepo." (takwimu hazijaoneshwa kwenye Kielelezo cha 1).

**Kielelezo cha 1: Kwa kiasi gani una imani na watu makundi haya?**




**Chanzo cha takwimu:** *Sauti za Wananchi,* Awamu ya 20, Juni– Julai 2014.


## Jambo la 2: Wananchi 7 kati ya 10 huomba ushauri kwa ndugu

Sauti za Wananchi iliwaliuliza wahojiwa juu ya namna wanavyofanya maamuzi muhimu katika masuala matatu (masuala ya jumla, masuala ya Serikali, masuala ya biashara), na wangeomba ushauri kutoka kwa nani.

Kwa masuala ya jumla (Kielelezo cha 2), Watanzania 72% waliripoti kuwa familia zao ni sehemu ya kwanza ya kutafuta ushauri. Kuomba ushauri kutoka kwa rafiki (66% walisema wanafanya hivyo) na Watanzania 53% walitaja majirani pia kama sehemu ya kupata ushauri (washiriki waliruhusiwa kutoa jibu zaidi ya moja).

Mbali na watu walio karibu nao, wananchi waliripoti kuwa wangeweza kutafuta mwongozo kutoka kwa viongozi wa dini. Hata hivyo, hakuna mtu aliyetaja sala (kuombewa) kama njia mojawapo ya ushauri. Wanasiasa walitajwa kwa kiasi kidogo sana kama chanzo cha ushauri, ikiwa ni wananchi 2 tu kati ya 10 (15%) waliosema hutafuta ushauri kutoka kwa wanasiasa. Wahojiwa hawakuulizwa kwanini walifanya maamuzi hayo, lakini kwa ujumla, kiwango cha mwitikio na aina ya ushauri unaotolewa vinaweza kuchangia kwenye namna watu wanavyofanya maamuzi haya.

**Kielelezo cha 2: Ndani ya kipindi cha miezi 12 iliyopita, je, ulitafuta ushauri ili kufanya uamuzi muhimu kutoka kwa yeyote kati ya watu hawa?**




**Chanzo cha takwimu:** *Sauti za Wananchi,* Awamu ya 20, Juni– Julai 2014.

Kwa maamuzi muhimu kuhusiana na Serikali, ni Watanzania wachache (33%) walio tayari kuomba ushauri kwa wazee waliopo ndani ya jamii (haijaoneshwa kwenye kielelezo cha 2). Hii inaibua maswali ya kuvutia: je, wazee mara nyingi hawafuatwi kuombwa ushauri kwa masuala ya jumla? Ni mwananchi 1 tu kati ya 4 ndiyo huomba ushauri kwa wazee, lakini wazee ni chanzo kikuu cha ushauri kwa Serikali.


## Jambo la 3: Mtanzania 1 kati ya 7 ndiye mwanachama wa chama cha siasa

Watanzania wengi (72%) ni wanachama wa mashirika ya kijamii. Mashirika haya ni pamoja na madhehebu ya dini, vikundi vya kuweka na kukopa, au chama cha siasa. Makundi maarufu zaidi ni asasi za kidini, ambapo wananchi karibu 4 kati ya 10 (36%) walisema wao ni wanachama wa kundi la dini (Kielelezo cha 3). Hata hivyo, pamoja na uwimbi wa siasa kusikika sana, 1 tu kati ya Watanzania 7 (16%) ndiye mwanachama wa chama cha siasa. Hii ina maana kuwa maoni yaliyokusanywa kupitia mifumo ya chama, kama vile mchakato wa mabadiliko ya Katiba, yanaweza kuwa ya uwakilishi wa Watanzania wachache tu.

Mbali na wananchi kupenda zaidi makundi ya kidini, watu wengi walionekana kuwa wamejiunga na makundi ya kiutendaji yanayohusiana na uzalishaji kipato na fedha kama vikundi vya kuweka akiba na kukopa (22%) vikundi vya biashara, kazi au makundi ya wakulima (19%).

Kwa ujumla, ushiriki wa mtu mmoja mmoja uliripotiwa kuwa mkubwa (kwa upande wa uanachama), kitu ambacho kiliashiria kuwa watu hawakushikilia tu uanachama "tupu" bali walitaka makundi yao yazae matunda mema. Hakika, watu wengi walionesha kuwa waliwahi kuhudhuria angalau nusu ya mikutano ya kundi walilojiunga nalo (Kielelezo cha 3).

**Kielelezo cha 3: Je, wewe ni mwanachama wa kati ya makundi, chama au vilabu vifuatavyo na unahudhuria mikutano yao?**




**Chanzo cha takwimu:** *Sauti za Wananchi,* Awamu ya 20, Juni – Julai 2014.


## Jambo la 4: Wananchi 84% wamewahi kutoa malalamiko katika makundi

Sauti za Wananchi iliuliza kuhusu aina ya hatua zinazoweza kuchukuliwa na mtu wakati anakabiliwa na tatizo, kuanzia kwenye hatua za kushiriki kama mtu "binafsi" kwa mfano, kulalamika kwa rafiki au kikundi juu ya suala la kijamii, hadi hatua ya kushiriki kama "umma", tabia kama kukataa kulipa kodi holela au kuhudhuria maandamano. Kwa kawaida Watanzania huwa wanashiriki zaidi kama umma; hii inaweza kuhusiana na wananchi kupenda au kutegemea muundo usio rasmi kuliko kufuata mfumo rasmi. Kielelezo cha 4 kinaonesha kuwa wananchi walisema wamewahi kusemea masuala yao (aidha kwa marafiki, vikundi vya jamii au kwenye hadhara) lakini hawako tayari sana kuchukua hatua zaidi.

Moja ya hatua inayochukuliwa sana na wananchi ni kulalamika kwenye kikundi kuhusu jambo ambalo halijakaa vizuri katika jamii; wananchi 8 kati ya 10 walisema huwa wanafanya hivyo (84%) (Kielelezo cha 4).

Watu pia walisema huwa wanapiga simu kwenye vipindi vya redio au kujihusisha kwenye baadhi ya mijadala ya umma (32%). Wananchi wanajihusisha kwa kiasi kidogo sana kuhudhuria maandamano, kukataa kulipa kodi, au kuwasilisha maoni kwenye sanduku la maoni.

**Kielelezo cha 4: Je, umefanya moja kati ya haya ndani ya kipindi cha mwaka mmoja uliopita?**





**Chanzo cha takwimu:** *Sauti za Wananchi,* Awamu ya 20, Juni – Julai 2014.

## Jambo la 5: Wananchi wengi hawajawahi kuwasiliana na wawakilishi wao

Karibu nusu (47%) ya wahojiwa walisema hawajawahi kuongea na mwenyekiti wao wa kijiji au mtaa katika kipindi ya mwaka uliopita (Kielelezo cha 5). Ikumbukwe kuwa, wawakilishi au viongozi hawa wanapaswa kuwa karibu na wananchi. Aidha, idadi kubwa wananchi hawajawahi kuongea mbunge wao (90%).

Vile vile, wananchi waliripoti kuwa hawajawahi kuibua na kupeleka jambo kwa kiongozi wao (83%), au afisa wa shirika lolote la Serikali (81%) ndani ya kipindi cha miezi 12.

**Kielelezo cha 5: Katika kipindi cha mwaka jana, ni mara ngapi umewasiliana na mmoja kati ya watu hawa kuhusu tatizo muhimu au kuwapa maoni yako?**




**Chanzo cha takwimu:** *Sauti za Wananchi,* Awamu ya 20, Juni – Julai 2014.


## Jambo la 6: Wananchi wengi hupeleka malalamiko kwa viongozi

Watanzania wengi – 6 kati ya 10 (58%) – waliripoti kuwa wameshawahi kupeleka malalamiko ya pamoja kwa viongozi katika jamii yao ndani ya miezi 12 iliyopita. Malalamiko haya kwa kawaida huandaliwa ili kudai maboresho kwenye huduma za umma ngazi za mitaa. Masuala yanayolalamikiwa sana ni pamoja na utoro wa mwalimu na upatikanaji wa maji safi na salama (Kielelezo cha 6).

Wananchi 2 tu kati ya 10 (23%) waliombwa na wanajamii wengine kushiriki hati ya madai ya kuchukua hatua (petition), lakini karibu kila mmoja (95%) aliyeombwa alikubali (au 22% ya sampuli nzima).

Licha ya wingi wa madai ya wananchi kwa Serikali kuchukua hatua ngazi za msingi, changamoto kubwa za utoaji huduma zinaendelea kuishamiri. Hii inaonesha kuwa madai ya wananchi kwa Serikali kuchukua hatua kwa kiasi kikubwa hayafanikiwi au kuwa ni hatua ndogo tu zinazochukuliwa kwa upande wa mamlaka husika.

**Kielelezo cha 6: Ndani ya miezi 12 iliyopita, ni mara ngapi wanakijiji/kitongoji walimfuata kwa pamoja kiongozi wa kijiji au kiongozi wa kisiasa kudai maboresho ya huduma ya jamii?**




**Chanzo cha takwimu:** *Sauti za Wananchi,* Awamu ya 20, Juni – Julai 2014.

## Jambo la 7: Watanzania 7 kati ya 10 (68%) huchangia ujenzi wa majengo ya umma – 4 kati ya hawa (39%) huwa wamelazimishwa


Wananchi hulipa kodi kwa Serikali, na hutarajia Serikali iwapatie bidhaa na huduma nzuri. Imekuwa kawaida kwa nakisi ya bajeti kufidiwa na misaada ya kimataifa au mikopo. Hata hivyo, vyanzo hivi vyote vya fedha havina uhakika: fedha za wafadhili zinaweza kuchelewa, na makusanyo ya mapato ya Serikali katika miaka ya hivi karibuni yamkuwa chini ya makadirio. Kwa mfano, mwaka 2013, Bunge liliidhinisha bajeti ya shilingi bilioni 312 kwa ajili ya kukamilisha miradi mbalimbali ya maji, lakini, mpaka Machi 2014, Wizara ya Maji ilikuwa imepokea shilingi bilioni 86 tu (asilimia 28% ya bajeti iliyopitishwa)[1].

Mapungufu hayo yanawafanya viongozi wa Serikali kuwaomba wananchi kuchangia moja kwa moja kwenye miradi ya maendeleo katika maeneo yao. Michango zinasimamiwa na jamii; hata hivyo, hakuna miongozo ya wazi kuhusu sera za uchangiaji, utaratibu wa ukusanyaji, ufuatiliaji wa matumizi ya fedha au taratibu rasmi za kudhibitiana. Hatua hii ya kuziba pengo la bajeti inaweza kuanzisha matatizo mapya: kutofautisha viwango, michango isiyolingana, na mianya mipya ya rushwa.


[1] http://www.ippmedia.com/frontend/?l=68485

Walipoulizwa kama walikuwa wamechangia muda wao au fedha kwa ajili ya ujenzi wa vituo au majengo ya umma (kwa mfano shule, barabara, kliniki za afya, vyoo vya umma), asilimia 68 walisema kuwa walichangia kwa kiwango fulani. Kati ya hao, asilimia 88 walisema walichangia fedha na asilimia 12 walitoa mchango wa muda wao. Tulipowadodosa zaidi kama uchangiaji huo ulikuwa wa hiyari, asilimia 61 tu ndiyo waliosema ulikuwa kwa hiari, na asilimia 39 walisema "walilazimishwa" (Kielelezo 7a na 7b).

**Kielelezo cha 7a: Je, ulichangia fedha au muda wako?**





**Kielelezo cha 7b: Uchangiaji wako ulikuwa wa hiari au wakulazimishwa?**




**Chanzo cha takwimu:** *Sauti za Wananchi,* Awamu ya 20, Juni – Julai 2014.

Ni jambo la kuvutia kuchunguza mahusiano kati ya michango na sifa ya mchangiaji. Mkazi aliyeishi muda mrefu kwenye jamii, ana uwezekano mkubwa wa kuchangia mara nyingi zaidi (takwimu hazijaoneshwa) ila wakazi wa mijini wana uwezo mdogo sana wa kuchangia. Watu wenye uwezo zaidi kiuchumi, walio kwenye asilimia 20 za juu huchangia mara chache sana (Kielelezo 8).

**Kielelezo cha 8: Uchangiaji wa huduma ya umma kwa kuangalia utajiri, maeneo uliko na elimu**




**Chanzo cha takwimu:** *Sauti za Wananchi,* Awamu ya 20, Juni – Julai 2014.

## Jambo la 8: Wananchi hawaoni kama wana ushawishi juu ya Serikali

Wananchi wamejibu kwa kukubali kauli nyingi zilizoorodheshwa kwenye jedwali la 1 kuhusu hisia binafsi zenye kuleta matokeo yanayotakiwa); zaidi ya asilimia 70 ya wahojiwa wamekubaliana na kauli zote. Kauli hizi nyingi ni chanya na zinahusiana na hisia za uwezo wao kufanya udhibiti juu ya maisha yao wenyewe.

Hata hivyo, wananchi pia wana mtazamo hasi kuhusu Serikali kushindwa kuitikia matakwa ya wananchi. Wanakubaliana kabisa na ukweli kuwa ushawishi pekee walionao juu ya Serikali ni kupitia kupiga kura (71%) na kwamba, masuala ya siasa ni magumu mno (83%). Hii inatoa ishara nzuri kuwa watu wako radhi na wana uwezo wa kushughulikia masuala wanayokabiliana nayo lakini wanakuta njia rasmi za kutafuta ufumbuzi au huduma kupitia Serikali kwa kiasi kikubwa hazipatikani kwao.

**Jedwali 1: Hisia za ndani na nje zenye kuleta ufanisi binafsi**

| Kauli dhahania | "Nakubali" au "Nakubali kabisa" |
|---|---|
| Nikijikuta kwenye matatizo, nitaweza kutafuta ufumbuzi | 93% |
| Nikijitahidi vya kutosha, nitafanikiwa kutatua matatizo yanayonikumba | 88% |
| Ni rahisi kwangu kubaki kwenye dira na kukamilisha malengo yangu | 87% |
| Hata kama mtu akinipinga, bado nitatafuta njia ya kupata ninachostahili | 87% |
| Nikiweka bidii ya kutosha, nitaweza kutatua matatizo yoyote magumu | 85% |
| Pindi ninapokabiliwa na matatizo, mara nyingi naweza kupata njia tofauti tofauti za kulitatua | 82% |
| Mara nyingi ninafanikiwa kushughulikia chochote kinachonikabili | 79% |
| Naamini ninaweza kukabiliana na matukio yasiyotarajiwa | 76% |
| Ninaweza kubaki mtulivu ninapokumbwa na magumu naamini uwezo wangu wakutafuta sululisho | 75% |
| Nashukuru uwepo wa vyanzo muhimu, nimefahamu namna ya kushughulikia hali nisizozitarajia | 72% |

**Chanzo cha takwimu:** *Sauti za Wananchi,* Awamu ya 20, Juni – Julai 2014.

**Jedwali la 2: Hisia zenye kuleta ufanisi binafsi katika masuala ya kisiasa**

| Kauli dhahania | "Nakubali" au "Nakubali kabisa" |
|---|---|
| Wakati fulani siasa na Serikali vinaonekana ni masuala magumu kiasi cha kwamba mtu kama mimi siwezi kuelewa nini kinachoendelea | 83% |
| Kupiga kura ni njia pekee ya watu kama mimi kupata sauti ya kuhoji ni jinsi gani Serikali inaendesha nchi | 71% |
| Watu kama mimi hatuna sauti yoyote kuhusu nini kile Serikali inafanya | 70% |

## 3. Hitimisho

Utafiti huu wa Sauti za Wananchi Twaweza umebaini kuwa Watanzania wanaamini kuwa wanao uwezo wa kutatua matatizo yao wenyewe na kuchangia katika masuala ya umma na kuungana kwa ajili ya kuboresha jamii zao; lakini wana imani ndogo na mifumo rasmi ya Serikali na wana uwezo mdogo wa kushiriki kikamilifu kudai mabadiliko kwa Serikali.

Viongozi na maofisa walio mbali na wananchi hawaaminiki, na kiwango cha wananchi kujiunga na vyama vya siasa kipo chini. Licha ya hayo, viongozi wa dini na Rais wanaonekana kuaminiwa na wananchi: asilimia 44 ya Watanzania wakiwa wemeonesha imani na Rais Kikwete. Aidha, Watanzania wanaziamini zaidi familia zao na wanajamii, na ushiriki wao katika masuala ya jamii ukiwa ni mkubwa.

Mawasiliano kati ya Watanzania, wawakilishi na wanasiasa wengine kwa ujumla ni mdogo. Mwaka uliopita (2013), wananchi zaidi kidogo ya nusu (53%) hawakuwahi kuzungumza na wenyeviti wa vijiji au mitaa na asilimia 90 hawakuwahi kuzungumza na wabunge wao. Hata hivyo, ushiriki kati ya wananchi wenyewe ni mkubwa, hasa kwenye masuala ya mijadala ya umma: wananchi 72% ni wanachama wa mashirika ya kijamii, wananchi asilimia 82 wameibua masuala ya kijamii wakiwa kwenye kundi la kijamii, na idadi ya kutosha walihudhuria mikutano ya kijamii, au kushiriki katika mijadala ya redio kwa kupiga simu au kushiriki mijadala ya umma. Aidha, wananchi karibu 9 kati 10 (86%) wameshiriki katika kushinikiza masuala ya kijamii kwa mwaka uliopita. Zaidi ya hayo, Watanzania asilimia 68 walitenga muda au fedha za kujenga au kukarabati majengo ya umma - ingawa, ni vema ieleweke kuwa, kati ya hao, asilimia 39 walisema kuwa walilazimishwa.

Hata hivyo, lilipokuja suala la uwezo wa raia kujituma kufanya jambo kwa uthubutu zaidi, Watanzania wengi hawakupenda kuzungumzia hisia au mawazo yao. Ni idadi ndogo sana ya Watanzania walioonesha kuwa waliwahi kushiriki maandamano au matembezi ya kupinga jambo fulani (8%).

Licha ya ushiriki mkubwa wa wananchi kwenye mijadala na kuchangia michango, utoaji wa huduma umebaki kuwa ni changamoto kubwa nchini Tanzania, huku hongo[2], utoro[3] kazini na usimamizi mbovu wa rasilimali[4] ukiendelezwa kwenye huduma mbalimbali za Serikali. Hii inahusiana na mwitikio duni wa mamlaka: shinikizo la madai ya jamii na mijadala ya jamii inaweza kuleta maboresho kama wahusika na wasimamizi wa huduma husika watakuwa tayari kusikia kero za watu na kuzishughulikia. Bila hatua madhubuti kuchukuliwa na mamlaka husika, ushiriki wa wananchi hautafanyiwa kazi. Na hivyo, mzunguko wa matatizo ya kutochukua hatua kwa upande wa watoa huduma, na kukosa imani na kushindwa kushirikiana na taasisi rasmi kwa upande wa wananchi, vinaweza kuwa sugu na nchi kushindwa kuendelea. Kuondoa mzunguko huu itahitaji kubadili mazoea, kwa wananchi kuanza kutambua na kudai haki zao kutoka kwa viongozi watakaosikiliza na kutekeleza matakwa ya wananchi.

[2] Twaweza, Agosti 2014. "Je, sheria, wakala na ahadi za kupambana na rushwa vimeleta mabadiliko?" Sauti za Wananchi

[3] Twaweza, Julai 2014. "Nini kinaendelea kwenye shule zetu?" Muhtasari wa Sauti za Wananchi. http://twaweza.org/uploads/files/Education-EN-FINAL.pdf

[4] Twaweza, Septemba 2013. "Akiba imekiwsha au ipo?" Muhtasari wa Sauti za Wananchi .http://twaweza.org/uploads/files/SzWAccesstoMedicinesBrief5190913EN.pdf